JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | **WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**

JARIDA MAALUM

# SHERIA BULLETIN

Toleo la 15



## Uzinduzi

# Kituo cha HUDUMA KWA MTEJA

**0262160360**


**BODI YA UHARIRI**

**ELIAKIM C. MASWI**
Katibu Mkuu

**LUSAJO MWAKABUKU**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**WAJUMBE**
William Mabusi | Hyasinta Kissima
**Msanifu Kurasa:** Lusajo Mwakabuku




*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Prof. Palamagamba John Kabudi akimsikiliza na kumhudumia Mwananchi aliyepiga simu katika Kituo cha Huduma kwa Mteja akitokea Wilaya ya Uyui Mkoani Tabora akiuliza kuhusu masuala ya usimamizi wa mirathi Septemba 5, 2024 wakati hafla ya uzinduzi wa Kituo cha Huduma kwa Mteja ikiendelea.*

**Na Lusajo Mwakabuku & Hyasinta Kissima**
- WyKS Dodoma

Wizara ya Katiba na Sheria imeanzisha Kituo cha Huduma Kwa Mteja kwa ajili ya Huduma za kisheria baada ya kubaini kuwa malalamiko mengi ya Wananchi yamekuwa yakiwasilishwa Wizarani kwa njia ya Barua au kufika moja kwa moja kwenye Ofisi za Wizara kwa kutumia gharama kubwa.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Kituo hicho Septemba 05, 2024 katika Ofisi za Wizara hiyo Mtumba Jijini Dodoma Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi amesema Kituo hicho kitawezesha kupokea Taarifa na malalamiko yanayohusu tuhuma za rushwa, ukiukwaji wa haki unaofanywa na Taasisi ama mtu mmoja mmoja, na maoni mbalimbali kutoka kwa wananchi kuhusiana na huduma zinazotolewa na Wizara ya Katiba na Sheria, pamoja na Taasisi zote zilizo katika mnyororo wa haki.

Aidha, kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia inayofahamika kama Mama Samia Legal Aid Campaign, ambayo ni kampeni inayolenga kuwasaidia wale wasio na uwezo wakumudu gharama za mawakili na wale walio pembezoni, kampeni hii imeleta hamasa kubwa kwa Wananchi ambao wamejitokeza kwa wingi kwalengo la kuwasilisha malalamiko na hoja za kisheria zinazohitaji ufumbuzi wa haraka.

Kituo cha Huduma kwa Mteja kitakuwa kinapokea malalamiko, hoja maswali na tuhuma za rushwa kwa njia ya simu kutoka kwa Wananchi kutoka maeneo mbalimbali ya nchi na kutatuliwa moja kwa moja na wataalam na hivyo kumrahisishia huduma mwananchi.

Prof. Kabudi alisema Wizara ya Katiba na Sheria ni miongoni Wizara vinara zinazotekeleza kwa vitendo falsafa za Rais Samia Suluhu Hassan za 4R, ambazo ni maridhiano, ustahilmilivu, mabadiliko na kujenga upya.

> **"Kituo hiki ni utekelezaji wa falsafa ya R Nne (4R) za Rais Samia Suluhu Hassan ambazo ni Maridhiano, Ustahimilivu, Mabadiliko na Kujenga upya, kupitia falsafa hizi Wizara inawezesha utatuzi wa migogoro, inatoa elimu na msaada wa kisheria" amesema Prof. Kabudi**



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne A. Sagini akizungumza kabla ya kumkaribisha Mgeni Rasmi wakati wa hafla ya kuzindua rasmi Kituo cha Huduma kwa Mteja. tarehe 05 Septemba, 2024.*

Amebainisha kuwa serikali iliamua kuanzisha kituo hicho ambapo Mwananchi anaweza kuwasilisha hoja yake kupitia namba ya simu 0262160360.

“Hii imesaidia kwa Wananchi wasio na uwezo wa kumudu gharama za usafiri kuja kuwasilisha malalamiko yao Wizarani, kwasasa Wananchi walio maeneo ya mbali sasa wana uwezo kuwasilisha malalamiko yao kwa njia ya simu kwenye kituo hichi na kufanyiwa kazi bila kufika wizarani,”amesema

Ameeleza kuwa takwimu za mwezi Februari hadi Agosti 31, 2024, malalamiko 499 yamesajiliwa na kati ya hayo 410 sawa na asilimia 82 yamefanyiwa kazi kikamilifu na 89 yapo hatua mbalimbali ya kutafutiwa ufumbuzi.

Aidha amesema wananchi wanakabiliwa na kero nyingi na kuanzishwa kwa kituo hicho ni dhamira ya serikali kutumia njia rahisi za kiteknolojia kuwafikia wananchi ili kutatuliwa kero zao kwa wakati.

“Wizara inampango wa kuongeza muda wa kutoa huduma uwe saa 24 na siku saba kwa wiki, niwashukuru wadau wa maendeleo FCDO kwa kufanikisha uwepo wa kituo hichi kwa kushirikiana bega kwa bega na Serikali,”amesema

Katika hafla ya uzinduzi huo, Prof. Kabudi amevitaka Vyombo vy Habari Nchini, kuendelea kuibua malalamiko na changamoto za Wananchi zinazohusiana na masuala ya Kisheria ili ziweze kushughulikiwa. Prof. Kabudi amesema kuwa, Vyombo vya Habari vimekuwa msaada mkubwa kwenye Jamii kwani vimekuwa vikitoa elimu kwa Wananchi ya namna wanavyoweza kutatuliwa changamoto zao.




*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Prof. Palamagamba John Kabudi akikata utepe ikiwa ni ishara ya kuzindua rasmi Kituo cha Huduma kwa Mteja. tarehe 05 Septemba, 2024 Mtumba Jijini Dodoma.*




## USAJILI WA MASHIRIKA YANAYOTOA MSAADA WA KISHERIA

Tembelea Tovuti ya Wizara ya Katiba na Sheria ya *www.sheria.go.tz*, kisha bonyeza eneo la Huduma Mtandao, kisha chagua Usajili wa watoa huduma za Msaada wa Kisheria.

Au ingia moja kwa moja kwenye anuani ya *https://legalaid.sheria.go.tz;* naNenda sehemu iliyoandikwa **REGISTRATION** kisha tengeneza akaunti ya Shirika kisha fuata maelekezo kusajili Shirika.



**"Kituo hiki kimeanzishwa baada ya Wizara kubaini kuwa malalamiko mengi ya Wananchi yamekuwa yakiwasilishwa Wizarani kwa njia ya barua au wananchi hao kufika moja kwa moja kwenye ofisi za Wizara kwa kutumia gharama kubwa za usafiri na kujikimu".**

*Jane Lyimo - Mkurugenzi wa Idara Katiba na Ufuatiliaji*




"Katika Mfumo huu wa kutumia Teknolojia hakika Vyombo vya Habari ni moja ya wadau wetu muhimu sana katika jamii. Natoa wito kwa vyombo vyote vya habari kuhakikisha kuwa wakati wote vinafikisha habari na elimu juu ya uwepo wa Kituo hiki kwa Wananchi ili Wananchi waweze kukitumia kituo hiki kupokea malalamiko. Nina amini tukiongeza Kampeni ya kuwaelimisha Wananchi juu ya uwepo wa kituo hiki tunaweza kupokea malalamiko mengi na kuweza kutatua changamoto nyingi zaidi ambazo zitawafanya Wananchi waweze kupungukiwa na changamoto ambazo zinawakabili. Endeleeni kuhabarisha umma na kuongeza nguvu na jitihada katika kutoa mrejesho kwa jamii ya namna malalamiko au hoja zinavyoshughulikiwa katika kupata haki zao" Alisema.

Mkurugenzi wa Katiba na Ufuatiliaji Haki, Wizara ya Katiba na Shearia, Jane Lyimo, alisema lengo la kuanzisha kituo hicho ni pamoja na kuboresha mifumo ya mawasiliano na huduma kwa umma.

Kadhalika, alisema ni matokeo ya programu ya kujenga taasisi katika kupambana na rushwa inayotekelezwa na wizara hiyo kwa lengo maalumu la kuziwezesha taasisi ikiwamo wizara katika kupambana na rushwa Tanzania na inatekelezwa kwa kushirikiana na idara maalumu ambayo inaratibu na kusimamia kituo hicho kutoa Ofisi ya Rais Ikulu kupitia ufadhili wa serikali ya Uingereza ambayo imewezesha uanzishwaji wa kituo hicho.

Alisema kituo hicho ambacho kimezinduliwa kwa lengo la kupokea taarifa za rushwa, hoja na malalamiko mbalimbali kutoka kwa wananchi, kilianza kufanya kazi Februari 21 mwaka huu baada ya kukamilika kwa usimikaji wa mfumo na vifaa mbalimbali vya kiteknolojia ya kisasa.

Mkurugenzi huyo alielezakuwa limetengwa eneo mahsusi ndani ya wizara hiyo ambalo limewekewa vifaa vya kisasa kwa ajili ya kituo hiki na tangu kuanzishwa kwake kituo kimemeendelea kupokea malalamiko kutoka katika kila pembe ya nchini na huduma zinatolewa na wataalamu wenye uwezo na uzoefu wa kutosha..

Kupitia kituo cha Huduma kwa Mteja, Wizara ya Katiba na Sheria imejipanga kuendelea kutoa huduma bora zaidi kwa Wananchi kwa kutambua kuwa Mawasiliano ya haraka na sahihi ni muhimu katika kuharakisha usawa, uwazi na haki katika jamii yetu.Uzinduzi wa Kituo hicho cha huduma kwa mteja utarahisisha kwa wale wenye malalamiko ya Kisheria kutoa taarifa ili waweze kusaidiwa.

**"Kuna eneo mahsusi limetengwa kwa ajili ya kituo hiki na tangu kuanzishwa kwake kituo kimemeendelea kupokea malalamiko ya wananchi kutoka maeneo mbalimbali nchini na huduma zinatolewa na wataalamu mahiri ambao wamejengewa uwezo,"** *alisema Bi. Jane.*



*Baadhi ya watunishi wa Wizara ya Katiba na Sheria wakifuatilia matukio mbalimbali yaliyokuwa yakiendelelea katika uwanja wa ofisi ya Wizara ya Katiba na Sheria Makao Makuu Mtumba jijini Dodoma wakati wa hafla ya kuzindua kituo cha Huduma kwa Mteja.*

# Matukio katika Picha



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Prof . Palamagamba John Kabudi akiwa ameambatana na Naibu Waziri Mhe. Jumanne Sagini wakipokelewa na Wakuu wa Idara na Vitengo kuelekea kuanza kwa hafla ya uzinduzi wa kituo cha Huduma kwa Mteja*




*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini akiteta jambo la Mkurugenzi wa Huduma za Kisheria Bi. Anjela Anatory.*



*Mkurugenzi wa Idara ya Haki za Binadamu Bi Nkasory Sarakikya akitoa neno la shukrani kwa niaba ya Watumishi wa Wizara.*

*Kikundi cha Ngoma asili cha Mchoya kutoka Wilaya ya Chamwino Mkoani Dodoma kikitoa burudani wakati wa uzinduzi wa Kituo cha Huduma kwa Mteja tarehe 5,Septemba 2024*





*Mwimbaji wa Nyimbo za kizazi kipya Jaquiline Mwarabu akitumbuiza wakati wa hafla ya uzinduzi wa Kituo cha Huduma kwa Mteja iliyofanyika Mtumba, jijini Dodoma.*

*Baadhi ya Wawakilishi wa Vyombo mbalimbali vya Habari jinini Dodoma wakifuatilia matukio yanayoendelea kwenye uzinduzi wa Kituo cha*





*Waziri wa Katiba na Sheria na, Naibu Waziri wakiwa katika picha ya pamoja na Watumishi wa Wizara.*